


MAMBO UNAYOPASWA KUJUA KUHUSU KUKEKETWA KWA WANAWAKE



<http://fgm.co.nz/where-is-fgm-practiced/>

Historia

- Takribani wanawake na wasichana milioni 200 duniani kote kwa wakati huu mara nyingi wanakabiliwa na madhara ya FGM, ambayo pia inajulikana kama Ukeketaji Kwa Wanawake au Tohara Kwa wanawake ikiwa zoezi hili limekita zaidi Asia, Mashariki ya Kati na Afrika. (www.who.int/mediacentre/factsheets/fs241)
- Kanada imepiga marufuku FGM - Ni Shambulio Lililozidi inayoadhibiwa kisheria

Utafiti

- **Uzima Women Relief Group International (Kikundi cha Msada cha Wanawake cha Uzima cha Kimataifa)** ilifanyautafiti kuhusu matatizo ya afya ya wanawake wa Kiafrika walioathiriwa na vitendo vya FGM
- Utafiti huu ulifanyika kati ya wanawake wa Kiafrika walio huko Toronto kutoka nchi za Afrika ambazo FGM hufanyika
- Lengo la utafiti lilikuwa ni kuchunguza masuala yanayohusu afya na masuala ambayo wanawake waliofanyiwa FGM wanapata na pia kutambua ufahamu wao wa sheria ya Kanada dhidi yake.
- Pamoja na kuhoji wanawake, maoni ya jamii na hali za watoa huduma zilihitajika

Matokeo ya utafiti

- Wanawake 21, watoa huduma 11 na viongozi 8 wa jamii walihojiwa.
- Wanawake 47% (10/21) waliohojiwa walisema kuwa FGM ni mada ya unyanyapaa na wanawake wengine wanaweza kuogopa kuifichua kwa watoa huduma wao

- Zaidi ya 90% (20/21) ya wanawake waliohojiwa wamepitia aina ya FGM iliyofanyika kati ya ujauzito na utuzima. Hii ni dalili kwamba wanawake wengi kutoka Afrika wanaishi wakiwa wameshuhudia FGM
- Wanawake wote walionyesha wasiwasi juu ya madhara yanayohusiana na kitendo hicho na kusema kuwa mengi ya madhara ni ya kudumu na hayawezi kubatilishwa
- Baadhi ya viongozi wa jamii walisema inafanyika kwa sababu za kitamaduni na za kidini
- Baadhi ya viongozi wa kidini katika jamii walisema kuwa maadili na nidhamu nzuri inaweza kuingizwa kwa njia ya elimu na ushauri bila kusababisha madhara ya mwili
- Washiriki wote walikubaliana kuwa kuna madhara makubwa yanayohusiana na FGM na walielezea wasiwasi kwenye afya ya wanawake na jamii nzima
- Kwa wanawake wote waliohojiwa, FGM ilifanyika nyumbani badala ya hospitalini.
- Sababu zilizotolewa kwa FGM ni pamoja na:
 - Mpito wa kuwa mwanamke
 - Kupunguza tamaa ya ngono
 - Kanuni ya Kitamaduni/Kidini ya kulinda wasichana ya kuhakikisha hali bora ya maadili muhimu kwa ndoa
 - Uamuzi wa familia

Masuala ya Kijamii:

- Kuzungumzia kuhusu FGM nje ya kikundi cha kitamaduni
- Aibu
- Ni vigumu kuchumbiana nje ya utamaduni kwa sababu ya unyanyapaa unaotokana na FGM nchini Kanada
- Unyanyapaa katika mahusiano
- Uzinifu unaofanywa na waume
- Talaka

Masuala ya Afya:

- Wanawake wote wameteseka kutokana na athari za FGM ikiwa ni pamoja na:
 - Maumivu makali ya kisaikologia yanayosababisha matatizo ya afya ya akili kama vile msongo wa mawazo na mfadhaiko.
 - Matatizo ya mfumo wa uzazi na mkojo
 - Kuvuja damu
 - Mshtuko
 - Matatizo wakati wa kujifungua
 - Kupungua kwa kuridhika kwa ngono
 - Hedhi chungu

Matatizo kwa huduma za afya:

- Ni vigumu kuwasiliana na Madaktari
- Wahuduma hawajaelimishwa kuhusu FGM
- Ukosefu wa ufahamu wa FGM ili kupinga kitendo hiki
- Kukosa kuridhishwa na watoa huduma kutokana na:
 - Saa za kusubiri
 - Madaktari hawana umakini wa kutosha

Mapendekezo ya Uzima Relief Group International (Kikundi cha Msaada cha Uzima cha Kimataifa)

- Elimu na ufahamu juu ya FGM inahitajika kwa jamii na watoa huduma
- Hatua zinazofaa zinapaswa kuchukuliwa ili kutekeleza sheria dhidi ya FGM
- Kupambana na ukandamizaji kwa njia ya moja kwa moja ili kuwawezesha wanawake
- Kunapaswa kuwe na ishara ya kuona na kampeni kuitia asasi za huduma za Afya ili kuonyesha kuunga mkono kwa haki za wanawake zinazohusu FGM
- Kunapaswa kuwe na mifumo ya usaidizi wa jamii kwa wanawake wa asili ya Afrika ili kuongeza fursa ya kushirikiana na kuzungumza kuhusu masuala ya kitamaduni

Utafiti huu ulifadhiliwa na



WOMEN'S COLLEGE HOSPITAL
Health care for women | REVOLUTIONIZED

<http://www.womensresearch.ca/>

Soma ripoti kamili katika tovuti za WCH na UZIMA



Uzima Women Relief Group International
Giving a new meaning of Life, hope and bright future to all women

www.uzimawomeninternational.org